



Yerusalemu Mpya

Jarida la Dunia

Mchungaji Tony Alamo

Makanisa Ulimwenguni Kote

Taifa la Kikristo la Alamo

Toleo 17800

TOFAUTI KATI YA WOKOVU NA DINI

na Tony Alamo

Katika ulimwengu huu, kuna watu wengi wa kidini kuliko waliookoka, waliozaliwa mara ya pili katika ROHO Biblia, kwa maneno mengi sana, hutuleza kwamba dini ni ya Ibilisi, lakini wokovu ni wa BWANA.¹

Tofauti kati ya kumwamini KRISTO na kuamini dini ni kwamba, kwa kumwamini KRISTO, MUNGU ndiye humtafuta mwanadamu. Kwa maneno mengine, ni MUNGU ambaye amemtafuta mwanadamu na bado amtafuta hadi sasa. Kwanza, MUNGU aliwasiliana kwanza na Adamu, Kaini, Sethi, Henoko, Nuhu, Ibrahimu, Isaka na Yakobo katika Agano la Kale. Katika Agano Jipy, kwanza aliwasiliana na Mathayo, Yohana na Mtume Paulo. Katika mwaka wa 1964, ALIWASILIANA nami, na kulikuwa na wenigne wengi tangu nyakati za Biblia hadi sasa. Kwa maneno mengine, MUNGU amewatafuta kondoo wote wa kiume, viongozi wa familia YAKE, akiwatuma ili waende kuwatafuta kondoo amba katika siku zijazo watakuwa wa mwisho kuokolewa, wale amba wataishi milele katika Ufalme wa Mbinguni pamoja na MUNGU BABA, KRISTO, MWANAWE wa pekee na ROHO MTAKATIFU milele yote.

KRISTO hutuagiza wafuasi WAKE, sisi sote, kuwatafuta wengine ili wawe wafuasi WAKE, ili nao wafanye vivyo hivyo.² Anafanya hivi katika Mathayo 28:18-20 kwa maneno yafuatayo: "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza [mkiwazamisha ndani ya maji mengi³] kwa jina la BABA, na MWANA, na ROHO MTAKATIFU; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Amen." Huyu ni KRISTO akimtafuta mwanadamu, lakini si mwanadamu akimtafuta MUNGU. Mwanadamu kumtafuta MUNGU ni "dini," lakini wakati MUNGU amtafutapo mwanadamu, ni "wokovu."

Dini zote humtaka mwanadamu ambaye hajaokoka amtafute MUNGU, au mwengine ye yote ambaye wanamdhania kuwa ndiye MUNGU. Dini ni nini? Dini ni imani ya mtu katika kile anachokidhania kuwa MUNGU na utii



Tony na Susan Alamo, bendi, na kwaya kwenye kipindi chao cha luninga [televisheni] miaka ya 1970 na mwanzo mwa miaka ya 1980.

wake kwa kitu hicho. Katika kila ufa-hamu wa mwanadamu kuna mungu wa aina fulani, lakini hakuna wazo la MUNGU mmoja wa kweli. Hii ndio sababu YESU, katika Mathayo 28:19, aliaambia wanafunzi WAKE wa wakati huo, wanafunzi wake wote hadi leo, "Basi, enendeni, MKAWAFANYE MATAIFA YOTE [nani aliye MUNGU wa kweli ambaye wanapaswa kumwabudu, na ambaye wanapaswa kumwabudu na kumtumikia YEYE pekee] kuwa wanafunzi, mkiwabatiza [mkiwazamisha ndani ya maji mengi] kwa jina la BABA, na MWANA, na ROHO MTAKATIFU."

Ili tuingie mbinguni, ni lazima tuwe wakamilifu.⁴ Twaweza kuwa wakamilifu kwa sababu MUNGU ametuamuru tuwe wakamilifu, na MUNGU kamwe hajatuamuru tuwe kitu ambacho hatuwezi kuwa.⁵ Katika Mathayo 5:48 YESU

(Inaendelea ukurasa wa 2)

¹ Isa. 1:11-16, 29:13-14, Yer. 7:8-11, 23:33-40, Eze. 13:1-23, Mik. 3:11, Mat. 6:5, 7-8, 7:21-23, 15:7-9, 21:28-32, 23:1-37, Lk. 6:46, 18:10-14, Yoh. 5:40, 6:35-58, 10:1-15, 14:6, 15:2, 2 Tim. 3:1-7, Tit. 1:16, Yak. 2:19 ² Dan. 12:3, Mat. 10:7-8, 28:19-20, Lk. 24:46-48, Mdo. 1:8, 2:38-41, 10:39-43, Rum. 7:4, 10:13-15, 1 Kor. 1:17-18, 21, 9:16-17, Efe. 3:2-10, Kol. 1:25-29, 2 Tim. 4:2, 5 ³ Mat. 28:19, Rum. 6:3-5, Kol. 2:10-12 ⁴ Kumb. 18:13, 1 Fal. 8:61, Zab. 119:1-3, Mat. 5:48, 2 Kor. 13:11, Efe. 4:11-13, 5:25-27, Flp. 3:12-15, Kol. 1:21-22, 1 Tim. 6:14, 2 Tim. 3:16-17, Yak. 1:4, 1 Yoh. 3:6-10, Ufu. 21:7, 27 ⁵ Mwa. 17:1, Law. 11:44-45, 19:2, 20:26, Kumb. 18:13, 1 Fal. 8:61, Zab. 15:1-5, 24:3-5, 119:1-3, Yoh. 17:17-23, Rum. 6:4-14, 8:1-14, 37, 2 Kor. 6:14-17, 13:11, Gal. 5:16, Efe. 4:11-13, 5:25-27, 6:10-18, Flp. 1:9-11, 2:12-15, 3:12-14, 4:13, Kol. 1:10-11, 21-22, 1 Thes. 4:6-7, 1 Tim. 6:11-14, 2 Tim. 3:16-17, Ebr. 2:18, 12:14, 13:20-21, Yak. 1:4, 27, 1 Pet. 1:15-16, 5:8-10, 1 Yoh. 2:14, 3:5-10, 4:4, Ufu. 3:1-5, 7:13-15

TOFAUTI KATI YA WOKOVU NA DINI

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 1)

asema, "Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama BABA yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu." Kama tunatembea katika ROHO MTAKATIFU, tu wakamilifu. Warumi 8:1-2 yasema, "Sasa, basi, haku na hukumu [hakuna Jehanamu, hakuna Ziwa la Moto] ya adhabu juu yao walio katika KRISTO YESU, wasio tembea katika mwili, bali katika ROHO. Kwa sababu sheria ya ROHO wa uzima ule ulio katika KRISTO YESU imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti."(Imenakiliwa kutoka kwa KJV). Tambua kwamba andiko hili halisemi tunaweza kuwa huru mbali na sheria ya ki-maadili. Tunaweza tu kuwa huru mbali na sheria ya dhambi na mauti. Sheria ya dhambi na mauti husema kwamba ikiwa tutavunja sheria ya ki-maadili baada ya kuzaliwa mara ya pili na ROHO, hakuna dhabihu (msamaha) nyininge zaidi kwa ajili ya dhambi. Waebrania 10:26-31 husema hili kwa namna hii, "Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; bali kuna kuitazamia hukumu yenyе kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wappingao [maadui wa MUNGU]. Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili au watatu. Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyeemkanyaga MWANA wa MUNGU, na kuihesabu damu ya agano aliyatokaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanya jeuri ROHO wa neema? Maana twamjua YEYE aliyesema, Kupatiliza kisasi ni juu YANGU, MIMI nitalipa. Na tena, BWANA atawahukumu watu WAKE. Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya MUNGU aliye hai." Hii ndiyo sababu kumcha BWANA ndio mwanzo wa hekima.⁶ Tunapaswa kufanya yale ASE MAYO, yaani kuka mbali na dini, na kuzaliwa mara ya pili na ROHO. Huu ndio ufahamu ANA OUTAKA kutoka kwetu, na

kumcha BWANA ni ufahamu.

Katika Yohana 3:5, YESU alimwambia Nikodemo ni LAZIMA azaliwe kwa ROHO. Kamwe YESU hakusema ni lazima ujiunge na dini fulani. Kumwamini KRISTO kamwe sio sawa na aina yoyote ya dini. Tena, kumwamini KRISTO ni MUNGU anakuja kumtafuta mwanadamu, akitamani mwandadamu amtumikie YEYE.

Mara nyangi watu huuliza, "Kuna tofauti gani kati ya Ukristo na dini?" Wanaweza kuuliza, "Je, Ukristo ni dini?" Ili kujibu swali hili kwa uaminifu, mimi ningesema Ukristo sio dini. Ukristo wa kweli ni wokovu. Ingawa Ukristo huchukuliwa na watu ambao hawajaangaziwa kiroho kuwa mojawapo ya dini kuu tano duniani, ukweli ni kwamba kumwamini KRISTO sio kuamini dini. Tunaweza pia kuelezea jambo hili kwa kusema kwamba, wale wanaomwamini KRISTO kwelikweli, ni Wakristo, na wala sio wafuasi wa kile kinachodhaniwa kuwa dini ya Kikristo. Hadi leo, dini zina historia ya ukatili dhidi ya Ukristo.

Kanisa la Kirumi la Katoliki liliwaua mamilioni ya watu katika nyakati tatu tofauti za mahakama za kanisa za kuzima uzushi. Na wamefanya mauaji mengine mengi katika kipindi cha miaka elfu mbili iliyopita, kama vile mauaji ya Waco, ambapo watoto wengi, pamoja na wazazi wao waliuawa. Vitendo vya aina hii vya Kanisa Katoliki la Kirumi

vinaendelea hadi wa leo.

Tunaweza kuangalia nyuma katika mahakama za kanisa za kuzima uzushi kule Uhispania, vilevile na vitendo vingine vya kinyama vilivofanywa na Vatican. Hii hujumuisha Wayahudi milioni sita waliouawa kule Auschwitz na katika kambi nyingine za mateso za wanazi. Vita vya sasa dhidi ya Ukristo vinakuja kutokea Vatican.⁷ Mamia ya mamilioni ya dola ya mali zetu kutoka kwa wengi wetu yalichukuliwa. Wamelazimika kuacha mali yao na wengi wetu ambao ni Wakristo wa kweli waliozaliwa mara ya pili tunatumikia vifungo vya maisha gerezani kwa mashtaka ya uongo kwa sababu ya dini ya Kikatoliki. Sizungumzii kuhusu wale wakongwe wa kike na kiume wa Kikatoliki ambao hushiriki shughuli za kishetani za kidini za Kanisa Katoliki la Kirumi. Hawa, hawana ufahamu wa mambo haya kama ilivyo kwa sehemu kubwa ya watu wanaosalia katika ulimwengu huu. Hata hivyo, haya ninayoyasema ni ukweli mtupu.

Wakati kengele za makanisa ya Katoliki na Kilutheri zilipokuwa zikilia huko Poland, mamilioni ya watu wasio na hatia waliuawa huko Ujeruman kwenye vyumba na majengo ya majiko ya gesi, kisha kuburutwa kwa buldoza na kumwagwa kwenye mashimo makubwa (makaburi ya watu wengi). Nimesimuliwa kwamba baadhi yao walikuwa wangali hai. Watazamaji waliyona haya

7 Dan. 7:7, 19-27, Ufu. 13:1-7, 17:1-18 8 Yer. 4:16, Danieli sura ya 4, Mat. 13:24-30, 36-43, 47-50, 24:29-31, Lk. 15:4-10, 1 Kor. 11:10, 1 Tim. 5:21, Ufu. 14:13-20 9 Kumb. 31:21, 2 Fal. 19:27, 1 Nya. 28:9, Ayu. 31:4, 34:21-22, 25, Zab. 44:21, 139:1-6, 12-16, Mith. 15:3, 11, Isa. 29:15-16, Lk. 16:15, Ebr. 4:13, 1 Yoh. 3:20 10 Mhu. 12:13-14, Dan. 7:9-10, Mat. 3:12, 24:3-15, 29-44, Mk. 4:22, Rum. 2:5-13, 16, 14:10-12, 2 Kor. 5:10-11, 2 Thes. 1:7-10, 2 Tim. 4:1, 8, Ebr. 10:30-31, Yud. 14-15, Ufu. 1:7, 11:18, 20:11-15

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

(Imetafsiriwa kutoka kwenye Kifaransa)

Tunahesabika kuwa waliokubaliwa na huduma yako!

Ujasiri ni kuwa na msimamo. Katika andiko hili inabaini kuwa u mpambanaji [askari] wa Kristo kwa namna unavyoiwasilisha serikali hii ya kipolisi ya mpinga Kristo. Jambo hili linathibitisha kwamba wewe ni shujaa. Nikutie moyo kidogo tu; wewe ni mshindi, na unaufahamu hili.

Tunakaribisha msaada wa kutupatia maandiko. Twawatakieni Pasaka njema Wakristo wote wa huduma ya Alamo.

Zigashane Maroyi Israel

Jimbo la Sud-Kivu, Jamhuri ya Kedemokrasia ya Kongo

yote na kuyasikia yote.⁸ MUNGU aliyaona yote, na MUNGU aliyasikia yote.⁹ Mshukuru MUNGU kwa ajili ya Siku ya Hukumu, ambayo iko karibu kuja.¹⁰

Luka sura ya 12, mstari wa 1-5 husema, "Wakati huo, makutano walipokutanika elfu elfu, hata wakakanyagana, [YESU] ALIANZA kuwaambia wanafunzi WAKE kwanza, Jilinden na chachu ya Mafarisayo [Wayahudi wenye kusika dini], ambayo ni unafiki [dhambi]. Lakini hakuna neno lililositirika ambalo halitafunuliwa, wala lililofichwa ambalo halitajulikana. Basi, yoyote mliyosema gizani yatasikiwa mwangani [na walini na MUNGU]; na mliyonena sikioni mwa mtu katika vyumba vya ndani, yatahubiriwa juu ya dari. Nami nawaambia ninyi rafiki ZANGU, msishaogope hao wauua mwili, kisha baada ya hayo hawana wawezalo kutenda zaidi. Lakini nitawaonya mtakayemwogopa; mwogope ni YULE ambaye AKIISHA KUMWUA

mtu ana uweza wa kumtupa katika Jephenum; naam, nawaambia, Mwogopeni HUYO [MUNGU MWENYE UWEZO WOTE]."

MUNGU alimjia Adamu, ambaye hakujua lipi la kufanya. MUNGU alimwambia ale matunda ya mti wa UZIMA ili aweze kuishi milele, lakini badala yake alikula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya amba MUNGU alimkataza asile.¹¹ Kwa mara nyingine, MUNGU alimjia Adamu na maarifa ya wokovu, lakini Adamu alichagua dini ya Shetani (ujuzi). Pia MUNGU huujia ulimwenguni wote na maarifa ya wokovu, ukiwamo na wewe, lakini kama kupe amba hung'ang'ania kwenye ngozi ya wanyama na binadamu, kuna uwezekano mkubwa wewe pia kung'ang'ania kwenye dini fulani ya Kishetani, sivyo?

MUNGU alimjia Sethi na maarifa ya wokovu, na kisha Sethi akaanza kumwabudu MUNGU. Kisha MUN-

GU akamjia Enoko ambaye alitembea na MUNGU, na MUNGU akamchukua mbinguni kuwa pamoja NAYE.¹² Kisha tena MUNGU akamjia Nuhu.¹³ Nuhu hakumjia MUNGU wala hata mmoja wa hao wengine. MUNGU alijwaja. Ibrahimu alikuwa mwabudu sanamu; mwanachama wa dini [fulani], lakini MUNGU alimjia. Ibrahimu hakumjia MUNGU.¹⁴ Musa hakumjia MUNGU; MUNGU alimtokea, na akamjia Musa.¹⁵ MUNGU alijwaja watu mamia wengine kama vile wanafunzi wa YESU. Alimjia Mtume Paulo, mtu wa dini, na kumfanya aokoke.¹⁶ Paulo akafanyika kuwa mwenye manufaa kwa MUNGU katika wokovu wake, akapigana vita vyema dhidi ya nguvu za giza ambavyo pia vilihuisha maandiko yake yenye wastani wa theluthi mbili ya Agano Jipyä lote. Haya yoye yalihusishwa katika wokovu wa kweli.

Katika kitabu cha Danieli, vijana watatu wa Kiebrania (Shadraka, Meshaki na Abednego) wote walitupwa katika tanuru ya moto kwa sababu hawakuabudu sanamu ya dhahabu ya mfalme – kwa sababu walikataa kuwa sehemu ya dini ya mfalme.¹⁷ "Ule moto ulikuwa hauna nguvu [juu ya miili yao], wala nywele za vichwa vyao hazikuteketea, wala suruali zao hazikubadilika, wala harufu ya moto haikuapata hata kidogo. Nebukadreza akanena, akasema, na ahimidiwe MUNGU wa Shadraka, na Meshaki, na Abednego; aliyemtuma malaika WAKE, akawaokoa watumishi WAKE waliomtumaini, wakaligeza neno la mfalme, na kujitoa miili yao ili wasimtumikie mungu mwingine [dini yoyote], wala kumwabudu, ila MUNGU wao wenye" (Danieli 3:27-28). Katika Agano Jipyä, Mtume Yohana alipitia uzoe fu uleule. Alichemshwa katika

(Inaendelea ukurasa wa 4)

14 Mwa. 12:1-8, 17:1-9, Mdo. 7:2-3, Ebr. 11:8 15 Kut. sura ya 3, Mdo. 7:29-34 16 Mdo. 9:1-22, Gal. 1:13-19
17 Dan. sura ya 3



HUDUMA YA MTANDAO YA ALAMO

www.alamoministries.com

¹¹ Mwa. 2:16-17, 3:1-6 ¹² Mwa. 5:22-24, Ebr. 11:5 ¹³ Mwa. 6:11-18, 22, Ebr. 11:7

Malawi

Kwa huduma ya Tony Alamo,

Kwanza kabisa, pokea salamu katika jina la Bwana Yesu Kristo. Natumaini na kuamini kuwa unaendela vema. Sisi huku, hatuna neno. Bwana anatuongoza mchana na usiku.

Tunaposambaza na kushuhudia kuhusu maandiko ya Tony Alamo, daima huwa tunaguswa na Roho Mtakatifu kama ilivyotendeka katika kitabu cha Matendo ya Mitume 1:8 na Marko 16:15-16, kwa sababu Mchungaji Tony alipewa kikamilifu nguvu na Mungu Mwenye uweza wote kuufikia ulimwengu wote kwa kupitia mahubiri kwa njia ya maandiko, yaani Biblia na vitabu. Hivyo tunapoeneza nguvu hizi kwenye mitaani, kwa hakika watu wengi wanamgeukia Mungu, kama vile Waislamu, Wahindu, Mashahidi wa Yehova, n.k., mijini, maeneo ya vijiji na pia katika magereza.

Hapa Malawi, tunamwombea mchungaji Alamo kila siku, ingawaje yumo kizuijini, siku moja ijayo, ataachiliwa katika jina la Bwana. Wanasheria wanabadilisha siku za kusikilizwa kwa kesi yake kila uchao, amepoteza uwezo wake wa kuona, lakini hapaswi kuogopa juu ya haya yote kwa sababu Mungu anaweza, na siku moja ataachana na nyakati hizi zote za mateso. Ayubu na Yusufu walipita katika baadhi ya nyakati za mateso. Yusufu aliuzwa na ndugu zake, lakini Mungu alimwinua. Kwa hiyo, kama serikali ya Marekani inampitisha Alamo katika nyakati za mateso, bado Mungu ndiye mwenye utawala. Siku moja, kila kitu kitakuwa shwari katika jina la Bwana.

Tunakuombea usiku na mchana pamoja na tunafunga mpaka Tony aachiliwe kutoka kizuijini.

Wenu katika Bwana,

Mchungaji Danileck Harry Mitepa

Huduma ya Tony Alamo, Jiji la Blantyre, Malawi, Afrika

TOFAUTI KATI YA WOKOVU NA DINI

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 3)

mafuta wala hakuungua. Wala hakufa kutohana na tukio hilo.

Ni ajabu kwamba katika Biblia yote, wakati wowote mwanadamu awapo na mawasiliano na MUNGU, ni kwa sababu daima MUNGU ndiye amewasiliana naye kwanza. Pia MUNGU alimtafuta Ayubu kwanza, na kisha Ayubu akamtimikia. Hakuna habari yoyote katika Biblia ambapo mwanadamu alimtimikia MUNGU kwa sababu kwanza alikuwa na mawazo ya kumtumikia MUNGU. Biblia nzima huzungumzia MUNGU ajaye kumtafuta mwanadamu. Siku moja, Isaya aliona maono na kusikia sauti ya BWANA ikisema, "...Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili YETU? Ndipo niliposema, mimi hapa, nitume mimi" (Isaya 6:8). Baada ya kuona maono, Yeremia alisimama kuwatabiria wana wa Israeli maneno ambayo YEHOVA alimwamuru kuenen (Yeremia 1:4-9). Pia Danieli aliona maono kabla ya hajaamua kuomba na kufunga, akimsihi YEHOVA kuurejeshi Yerusalem (Danieli sura 7-9). Biblia nzima huonesha kwamba MUNGU humjia kwanza mwanadamu kabla mwanadamu hajamtumikia MUNGU.

MUNGU anawasiliana nawe kuitia kwangu na wachungaji wengine ambao wameokoka na wainjilisti, na kwa hivyo hauna udhuru. ROHO wa MUNGU, ambaye anaishi na kutenza kazi ndani yetu na kuitia kwetu sisi ambao tumeokoka, anakutafuta, awasiliane nawe, sio kwa ajili ya dini, bali kwa ajili ya wokovu wako na wokovu wa wengine.

Warumi 10:12-15 husema waziwazi kwamba wahubiri watumwao na MUNGU lazima wapelekwe duniani kote ili watu wauamini wokovu kwa kutumia maneno haya: "Kwa maana hakuna tofauti ya Myahudi na Myunani [mtu wa mataifa]; maana YEYE yule ni BWANA wa wote, mwenye utajiri kwa wote wamwitao; kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la BWANA ataokoka. Basi wamwi-

teje YEYE wasiyemwamini? Tena wamwaminje YEYE wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyo-andikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema!"

Kwa mara nyininge, YESU ametutuma kwako. MUNGU anakutafuta; sio wewe unayemtafuta MUNGU. Ukweli huu umelezwa kwako katika Luka 10:1-12 ambayo husema, "Basi, baada ya hayo BWANA aliweka na wengine, sabini [wanafunzi], akawatuma wawili wawili WAMTANGULIE kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda MWE-NYEWE. AKAWAAMBIA, mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache; basi mwombeni BWANA wa mavuno APELEKE watenda kazi katika mavuno YAKE. Enendeni, angalieni, NAWATUMA kama wana kondoo kati ya mbwamwitu. Msichukue mfuko, wala mkoba, wala viatu; wala msimwamkie mtu njiani. Na nyumba yoyote mtakayoingia, semeni kwanza, Amani iwemo nyumbani humu;

na akiwamo MWANA wa amani, amani yenu itamkalia; la, hayumo, amani yenu itarudi kwenu. Basi, kaeni katika nyumba iyo hiyo, mkila na kunywa vya kwao; maana, mtenda kazi amestahili kuperwa ujira wake. Msihame-hame kutoka nyumba hii kwenda nyumba hii. Na mji wowote mtakaouingia, wakiwakaribisha, vileni vyakula viwekwavyo mbele yenu; waponyeni wagonjwa waliomo, waambieni, Ufalme wa MUNGU umewakaribia. Na mji wowote mtakaouingia, nao hawawakaribishi, tokeni humo, nanyi mkipi-ta katika njia zake semenii, Hata mavumbi ya mji wenu yaliyogandamana na miguu yetu tunayakung'uta juu yenu. Lakini jueni hili, ya kuwa Ufalme wa MUNGU umekaribia. Nawaambia ya kwamba siku ile itakuwa rahisi zaidi Sodoma kuistahimili adhabu yake kuliko mji huo."

Wale wanaoiamini dini huchukua jukumu la kutumikia kile wanachokidhania kuwa ni mungu, wakati wale wanomwamini KRISTO humtumikia MUNGU baada ya kushawishiwa na

Haiti

(Imetafsiriwa kutoka kwenye Kifaransa)

Mpendwa Mchungaji Tony Alamo, mtumishi wa Mungu,

Bwana Yesu akusaidie zaidi katika kila nyanja ya huduma yako, hususan katika uinjilisti ili uweze kuzileta nafsi kwa Yesu kutoka pande zote ulimwenguni. Tunashukuru sana kwa kifurushi cha maandiko, (yaani vitabu vya Masihi na Biblia) ambavyo ultutumia, ili kutusaidia kueneza Injili ya Yesu Kristo na kuifanya inawiri. Asante. Mbingu haiko tupu na Mungu amezingatia jambo hili. Mapema tu, kikundi cha Groupe Fiancée De Christ kitakutumia jambo la kukushangaza kwa njia ya barua ili kukutia moyo katika kazi ya Bwana Yesu. Tafadhali tujulishe punde tu utakapopata ujumbe huo wa kukushangaza.

Tunataka kusambaza maandiko katika mtindo wa kufanya uinjilisti katika tarehe zifuatazo: 1, 2, 7, 8, na 10 za mwezi Aprili 2013, ambazo tumeziita: Kampeni Kubwa ya Uinjilisti katika mji wa Pont-Rouge. Kutakuwa na siku mbili za mikutano ya hadhara itakayohusisha vyombo vya kupaza sauti, na siku tatu za kueneza injili ya Kristo. Tafadhali tukumbuke kwenye maombi, kwani Shetani anapambana nasi, lakini ushindi ni wetu. Tutakapomaliza maandiko haya tutakujulisha ili ututumie tena.

Tunaendelea kukuombea, na usihofu, kwani umefichwa ndani ya Kristo. Ushindi ni wako na kwa familia yako.

Wakati wote dumu katika utakaso, katika maombi, katika kufunga, na katika upendo wa ndugu. Jiokoe kutoka katika kizazi hiki cha upotevu.

Cesar Francis Junior

Mratibu Mkuu (Groupe Fiancée De Christ)

Pont-Rouge, Haiti

kuguswa na MUNGU. Kwa sababu hii, ninasema kwamba mtu yeoyote hapaswi kuwa na haraka ya kumtumikia mungu ambaye ni kitu cha kubuni tu, yaani kumtumikia dini tu. Twamtumikia MUNGU tu wakati YEYE, kwa ROHO WAKE, yu ndani yetu.¹⁸ Ikiwa tutamtumikia MUNGU bila YEYE kwanza kuishi ndani yetu, tuko ndani ya dini na wala sio ndani ya wokovu. Tukiongea kwa mafumbo, watu wengi leo wanabandika bango la "Mkristo" kwa nje, lakini kwa ndani wanahusika na biashara za kidini. Wao ni Wakristo katika akili zao wenyewe, lakini katika uhalisia wao ni wanadini tu.

Kuwa Mkristo ni nini? Mkristo ni mtu ambaye KRISTO anaishi na kuten-da kazi ndani yake kwa njia ya ROHO

MTAKATIFU, naye huendeshwa na ROHO MTAKATIFU ili kumtumikia MUNGU.¹⁹ Kwa upande mwininge, mtu wa kidini ni yule anayeamini ya kwamba anamtumikia mungu na kutamani kutenda yale ambayo anadhani huyo mungu angemtaka ayafanye. Hii ndio hali ya watu wengi wanaokiri kuwa Wakristo leo. Wanaokiri Ukristo, lakini hawajazaliwa mara ya pili. Hawajaokolewa, kwa hiyo hawamjui KRISTO, na hawana ufhamu wa jinsi ya KUMTUMIKIA. Hawawezi kumfuata KRISTO kwa sababu hawawezi KUMSIKIA.²⁰ Kwa hiyo, wanatenda mambo kwa mapenzi yao, na MUNGU wa kweli hawezi kuwatumia. Hawafai. Walakini, kwa uzofu wa wale walio Wakristo wa kweli, BWANA

¹⁸ Eze. 36:27, Yoh. 14:15-20, 23, 26, 15:1-11, 26, 16:7-14, Rum. 8:1, 10-11, 26-28, 1 Kor. 3:9, 16-17, 6:19-20, 2 Kor. 6:16-18, Efe. 2:18-22, Flp. 2:12-13, Kol. 1:27-29, 2 Tim. 1:14, 1 Yoh. 4:4, 5:12 ¹⁹ Isa. 30:21, Yoh. 15:1-5, 17:21-23, 26, 1 Kor. 15:10, 2 Kor. 5:17-21, Gal. 2:20, Efe. 3:16-21, 1 Yoh. 2:20, 27 ²⁰ Yoh. 8:42-43, 10:27

NDIYE awaongozaye katika mambo yote. Kwa urahisi wao husema, "Ndio. Amina." BWANA ndiye kiongozi wao na MUNGU wao. Hii ni tofauti kabisa na njia ya watu wa kidini.

Baada ya Mtume Paulo kukutana na BWANA kwenye barabara ya kwenda Dameski, maneno ya kwanza aliyozungumza yalikuwa, "U nani WEWE, BWANA?" (Paulo alifahamu kuwa ali-kuwa ni BWANA, kama sivyo asingeuliza, "U nani WEWE, BWANA?") Kisha BWANA akamwambia, "MIMI ndimi YESU unayeniudhi wewe [Pindi mtu yeoyote amtesapo mshiriki wa kanisa la KRISTO, anamtesa KRISTO. Hii ni kwa sababu sisi ni mwili WAKE, heka-lu LAKE, yaani Mwili wa KRISTO]." 1 Wakorintho 3:16-17 hutuambia hivi, "Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la MUNGU, na ya kuwa ROHO wa MUNGU anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la MUNGU [Mwili wa BWANA, ambao ndio sisi], MUNGU atamharibu mtu huyo. Kwa maana heka-lu la MUNGU ni Takatifu, ambalo ndilo ninyi." Ni Takatifu kwa sababu hamfuati dini mfu, ambayo kwayo KRISTO na BABA, kwa njia ya ROHO haishi ndani yake, lakini wewe ni Mkristo uliyezaliwa mara ya pili. KRISTO kwa njia ya BABA na kwa njia ya ROHO, huishi ndani yako, kama umeokolewa, u hekalu la MUNGU. Hii ndio sababu MWILI ambao MUNGU anaishi ndani yake ni Mtakatifu, na mwili ambao MUNGU haishi ndani yake sio Mtakatifu ila ni najisi. Kwa hakika utataka kuwa Mtakatifu zaidi kila kitu wakati utakaposimama kwenye Kiti cha Hukumu cha MUNGU.

Dunia imejaa vikwazo na vizuizi. Hivi ni vikwazo vya Shetani vinavyofanya akili yako kukosa mwelekeo kwenye jambo lililo muhimu kabisa katika ulimwengu huu, ambalo ni kuidumisha roho yako katika kumtumikia MUNGU na kumdumisha KRISTO na BABA YAKE kuishi ndani yako. "Mwacheni mwanadamu ambaye pumzi yake i katika mianzi ya pua yake; kwa maana hudhaniwaje kuwa ni kitu?" (Isaya 2:22).

Chagua jambo moja: je, unataka kuwa MWILI Mtakatifu wa MUNGU, au un-

(Inaendelea ukurasa wa 8)

Arkansas

Mchungaji Tony,

Vera ambaye ni meneja wa hoteli kutoka kule New Orleans, alinipigia simu siku chache zilizopita. Huyu ndiye aliyewasaidia ndugu wa kike na wa kiume kila wakati ilipohitajika, kwa mfano, wakati ule walipohitaji kufanyiwa upasuaji na walipok-wenda hospitalini huko New Orleans.

Vera hajawahi kusahau ushauri uliompa wakati alipokuwa na shida nydingi na wafanyakazi wake wa hoteli. Ulimwambia, "Kwa nini usiwaajiri Wakristo ambao wanahitaji kazi nzuri kisha ninyi nyote mnaweza kutamtufuta Bwana kwa pamoja? Naamini biashara yako itanawiri." Bila kusubiri, Vera aliyutilia maanani ushauri wako, na mara akawa na wafanyakazi Wakristo wanaoiamini Biblia, ambao hukutana pamoja kila siku hotelini kabla ya kuanza kazi, wakisoma Biblia na kuomba pamoja.

Mujiza ultendeka – kila mmoja alifanya kazi kwa bidii, wakisafisha na kuweka vitu vema kwa furaha, na biashara ya hoteli ile ikaanza kustawi mpaka wakapewa tuzo kutoka ofisi ya Mkuu wa eneo hilo.

Bwana alimwamsha Vera mnamo majira ya saa saba usiku, usiku ambao Kimbunga cha Katrina kiliukumba mji wa New Orleans. Bwana alimwambia achukue nguo na matumizi kidogo aweke kwenye gari kisha yeye na mume wake wakimbilie kwa Jackson, huko Mississippi, "SASA HIVI, HARAKA!!!!" Yeye na mume wake, usiku ule walikuwa kwenye hoteli kwa sababu nyumba yao kule Gulfport ilikuwa imeuzwa.

Si tu kwamba Mungu aliyao kwa maisha yake wakati huo, lakini pia mama huyu ni manusura wa saratani ya matiti. Kama ulivyosema Mchungaji Tony, alipanda mbegu ya huruma kwa kuwashughulikia ndugu wa kike na wa kiume ambao walikuwa na mahitaji kwa miaka mingi, naye Mungu akamhurumia.

Huwa anasikiliza jumbe ambazo Mungu amekupa kwenye CD na alitaka kwa hakika ujue kwamba anakupenda katika Bwana, na anakuombea, na anaamini Mungu atatenda tendo kuu kwa ajili yako kwa sababu wewe ni wa Bwana, na ume-panda rehemaa nyingi sana.

Bwana asifiwe.

Merry Anne

Texarkana, Arkansas

India

Ndugu Wapendwa katika Kristo,

Nawajulisheni kwamba, kwa utukufu wa Mungu, mikutano yetu ilimalizika kwa miujiza ya ajabu. Zaidi ya washiriki elfu moja walihudhuria. Wakati wa mikutano hii, niligawa maandiko yako kwenye kusanyiko hili kubwa, na washiriki wengi walimpokea Bwana.

Utukufu ni kwa Bwana. Kila mmoja aliiombea kesi ya Mchungaji wetu. Tuombeenii pia.

Ndugu yenu mpendwa,

Solman Raju Kola

Andhra Pradesh, India



Ufilipino

Asante sana Mchungaji Tony, kwa makala hii ya ajabu, "Kusaga na Kukereza Meno." Utukufu ni kwa Mungu! Naipenda sana kwani inajumuisha nidhamu.

Nidhamu inahitajika sana leo kwa Wakristo duniani kote.

Mchungaji Cecilio H. Asis, Jr.

Albay, Ufilipino



Darakonda Vidya Sagar akigawa maandiko ya kuwaleta watu kwa Yesu ya Mchungaji Alamo, yaliyotafsiriwa kwa lugha ya Telugu, vijijini na mijini kuzunguka mji wa Visakhapatnam, Andhra Pradesh, India.

Kalifornia

Kwa Ndugu zangu katika Kristo,

Natumaini nyote mu wazima katika Kristo. Daima huwa ninabarikiwa sana kupata habari kutoka kwenye timu inayohusika na barua-pepe. Ahsante kwa kuendelea kuniombea. Hakuna siku ambayo hupita bila kuwataja kwenye maombi yangu, hususan Mchungaji Tony. Leo ni meipokea boksi la maandiko mbalimbali na nikajawa na furaha wakati nilipoona aina tofauti nyingi za maandiko ambayo sikuwa nayo hapo awali. Kwa kweli ili-kuwa kama kupokea zawadi ya Krismasi. Niliweza kumhisi Mungu kwenye maandiko haya. Nilichukua kwa haraka makala iitwayo, "Mungu hana Mama" na kisha nikaanza kusoma kwa sauti kubwa ili kila mwenye sikio, asikie. Utukufu kwa Mungu.

Si zaidi ya wiki moja iliyopita nilikuwa nikimwambia mke wangu kuhusu gharma ya mafuta ya gari kwa sasa kwenda kanisani huko Los Angeles. Kupata mwali-liko wako, ni jambo jema, nitaufanya kazi. Hapo awali safari moja ya kwenda na kurudi iligharimu dola za Marekani 100, laki-

ni sasa imepanda hadi dola 200 kwa safari moja ya kwenda na kurudi; lakini najua kwamba Mungu wa miungu na Bwana wa mabwana wote atafungua mlango kwa namna yoyote akipenda. Asante kwa mwali-liko huo. Sauti ya Mungu iliponiambia nifungashe mabegi yangu kwa muda wa wiki tatu na kwenda kanisani nilitii, nilibarikiwa kuwa Mkristo ninayetembelea watu hapo nyuma, na ilikuwa, na bado ni uzoefu bora kabisa wa kiroho niliopata kukutana nao. Nyimbo zenyewe zilikuwa nzuri sana, na nilimhisi Mungu akitembea kwenye kila ibada. Niliweza kumhisi Mungu wakati nikiendesha gari langu nikipita kwenye bonde lililo karibu na kanisa, na ningetamani kweli kuwa na uzoefu kama huo tena. Bila kusahau, chakula kilikuwa kitamu sana, kusikia shuhuda zote, kufanya kazi pamoja na ndugu kwenye mitaa na kuona jinsi mambo yanavyofanywa. Jinsi walivyojibu kila swali wakitumia neno la Mungu, hapo ndipo nilipojua kuwa ninataka kile walichonacho. Sasa,

baada ya miaka kadhaa, na baada ya kusoma kwingi, niko karibu kuwafikia.

Basi, jambo la kwanza ambalo papa wao mpya maarufu alisema kwa umati wa watu ni kwamba anakwenda kuomba kwa Bikira Mariamu. Ongea kuhusu kipofu kumwongoza kipofu kuingia kwenye shimo! Aisee! Kwa namna ile ile ni zaidi sana. Hii ndiyo sababu nilifikiri ingekuwa sahihi kusoma "Mungu hana Mama." Mchungaji wakati wote huwa hakosei kuhusu fedha katika maisha yangu. Nina shuhuda ambaa ningependa kuwashirikisha ninyi nyote kuhusu UFO, na Mchungaji na Suzie na jinsi hayo yote yalivyofanyika bayana katika maisha, nitafanya hivyo kwenye barua yangu ijayo. Namwomba Bwana awabariki nyote na kila siku awalete kondoo wengi zaidi zizini kwa namna mfanyakavyo kwa jinsi ya kushangaza sana.

Utukufu kwa Bwana.

Usiku Mwema.

Ndugu Tom C.

Kalifornia

Zambia

Mpendwa Mchungaji,

Acha nianze barua hii kwa kuitambua kazi ambayo Bwana Yesu Kristo amekuitia. Mara ya kwanza kupokea maandiko ya Biblia kutoka katika kanisa lako ilikuwa mwezi Juni 2012. Kwa jumla nilipokea majorida 382 pamoja na maandiko mengine, vitabu sita vya *Mashihi* na Biblia moja ya toleo la King James. Kazi nzuri ilijojo! Hili lilikuwa jambo la kufurahisha kuptita kikomo na la ajabu! Sina maneno ya kutosha kuelezea shukrani zangu, lakini Mungu ajuaye yote ni shahidi wangu ni kwa kiasi gani maandiko yako yenye uvuvio yalichokifanya maishani mwangu na katika maisha ya wale waliogawiwa.

Wakati wowote Bwana aliponipa nafasi na muda, maandiko yaliweza kugawiwa kwenye mabweni ya wanafunzi, ndani ya mabasi, wakati mwingine nilipokuwa katika safari zangu mitaani, mabarabara, sokoni, n.k. Hili pia liliwezekana wakati wa kufanya uinjilisti au wakati wangu binafsi wa kuwatemebelea watu.

Baadhi ya marafiki zangu (ndugu katika Bwana) walipata vitabu vya *Mashihi* na maandiko mengine ya kutumia kwenye kazi ya uinjilisti mahali popote ambapo Mungu angewatuma kwa wakati huo au mwingine. Kwa urahisi, hili humaanisha kwamba, kwa jinsi maandishi yako yaliyovuviva yalivyoweza kufikia sehemu mbalimbali za dunia, Ewe mtumishi wa Mungu, vivyo hivyo nasi twaomba na kuamini kwamba maandiko haya hayana budi kusambazwa kikamilifu ndani na nje ya nchi yetu (Zambia). Ndio! Wale wanaosoma na kuamini vazi la neema lilolelezwa bayana kwenye maandiko yako kumhusu Yesu Kristo, kwa hakika wataokoka!

Mtumishi wa Mungu, ninaweza kushuhudia kwamba siri za upendo wa Mungu ambazo zimeelezwa kinagaubaga katika maandiko yako, zinadhiirisha wazi kwamba wewe sio tu mchungaji na mwinjilisti anayewaka moto wa Roho Mtakatifu ili kumfanya Mungu agawe uhai wake kwa wenigne. Wengi waliosoma maandiko yako wamerudi wakishuhudia nguvu zilizo katika maandiko ya Mchungaji Alamo. Wanafunguliwa macho na kutolewa ujinga na kisha kujazwa hekima ili watilie mkazo mambo ya kwenda mbinguni.

Mungu mkuu aliyejuita kutenda kazi hii njema na anayeyashikilia maisha na mienendo yetu katika mkono wake wa uweza (Danieli 5:23), akutie nguvu na bila mawaa hadi siku ya kufunuliwa kwake Mungu wetu mkuu na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Amina (Yuda 24-25, Tito 2:11-15, 1 Wakorintho 1:7-9).

Kwa hivyo, sasa natuma maombi mapya ya kutumiwa maandiko yako yenye upako kwa miaka ijayo ikiwa kanisa lako lina uwezo wa kutuma kulingana na idadi iliyoonyeshwa. (Orodha ya maandiko imeondolewa)

Jitihada na utayari wenu wa hali ya juu utaheshimika sana.

Wenu katika mwito mkuu wa Yesu Kristo,
Zimba Moses

Lusaka, Zambia

New York

Tony ni mtu mwema wa Mungu. Nimemfahamu kwa miaka 43. Mungu ambariki. Nilimjua Tony Alamo kibinagsi. Tony yuko sawa kuhusu Kanisa Katoliki na amepitia mateso mengi mno kwa sababu ya kuongea kuhusu kanisa hilo, na pia kwa kuwa yeye ni Myahudi wa Kimasihi kwa ajili ya Kristo. Tony ni mtu mwema wa Kristo na amekuwa akigandamizwa sana na nguvu za kishetani kwa sababu ya imani yake kwa Kristo. Sote hatuna budi kumuombea. Mungu akubariki, Tony, kwa msimamo wako kwa Yesu na kwa msimamo wako kinyume cha uovu wa shetani.

Ted Whitus

NY, NY

Australia

(Imetafsiriwa kutoka kwenye Kihispania)

Kwa ndugu Tony Alamo,

Ndugu mpendwa katika Kristo, kwa kweli niliipenda sana tovuti yenu na ninakubaliana kabisa na matamko yako. Naamini huu ni wakati wa kuyachimba zaidi maandiko.

Tafadhali nakuomba unitumie kitabu cha *Mashihi*, ambacho kinajumuisha nabii 333. Pia, ikiwa una aina nydingine yoyote ya video au kitabu kuhusu mada hizi ambazo ni muhimu sana, tafadhali watumie waumini.

Asante sana, nitaiombea huduma yako katika kutangaza kweli hizi.

Baraka katika Kristo,

Beatriz Martinez

Ferntree Gully, Victoria, Australia

New Mexico

Miaka kadhaa iliyopita, Peter Hernandez alikuwa gerezani, akiwa mganjwa sana mwenye uvimbe kwenye ubongo. Madaktari walimwambia ya kwamba alikuwa na siku tisini za kuishi. Alimwandikia barua Mchungaji Alamo ambaye aliwasiliana naye, akaiimarisha imani yake, na kumtia moyo Peter aineue imani yake na kudai uponyaji wake. Kanisa lote lilimwombiea. Baadaye Peter aliandika barua ya majibu yenye shukrani kwa sababu alisema Bwana alimtumia Mchungaji Alamo kwa namna yenye uwezo na akaponywa. Peter anaendelea kutembea kwa ushindi bila athari yoyote ya uvimbe kwenye ubongo ambaa ulikuwa na ukubwa wa mpira wa gofu. Bwana alimponya kwa asilimia mia moja, na muda mfupi baadaye, alipewa ruhusa na kutoka hospitalini na kujinga na mke na mtoto wake wa kike.

Wakati alipokuwa akigawa maandiko ya injili huko Las Cruces, New Mexico, hivi majuzi, wanandoa kutoka kanisani walikutana naye bila kutarajia. Aliwaambia jinsi Mchungaji Alamo daima alivyowasaidia watu waliokuwa na shida, alivyosaidia familia yake (Peter), akituma nguo na kuipa familia yake mahali pa kuishi kanisani wakati yeze Peter alipokuwa gerezani. Peter alisema kwamba Tony alimsaidia wakati wa uhitaji wake. Peter alisema alitaka kuwa sehemu ya huduma ya Tony na kanisa kwa kumpa ushauri na huduma za kisheria kwa shughuli zake, na anataka kugawa maandiko ya injili katika eneo lake.

Uingereza

Wakati ndugu Tony anapoongea, Vatican huanza kutetemeka mpaka kwenye viatu vyao. Ndugu Tony, umemfanya Shetani kujimbia katika jina la Yesu, Amina.

Jonathan Bailey

Newcastle, Uingereza

TOFAUTI KATI YA WOKOVU NA DINI

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 5)

ataka kuwa mwili mwingine tu wowote ulio najisi ambao ndani yake Shetani hukaa? Ikiwa chaguo lako ni kuwa MWILI wa KRISTO, omba sala hii:

BWANA wangu na MUNGU wangu, ihurumie roho yangu, mimi mweenye dhambi²¹ ninaamini kwamba YESU KRISTO ni mwana wa MUNGU aliye hai.²² Ninaamini kwamba aliku-fa msalabani na kumwaga damu yake ya thamani ili nisamehewe dhambi zangu zote nilizozifanya hapo awali.²³ Ninaamini kwamba Mungu alimfufua YESU kutoka kwa wafu kupitia nguvu za ROHO MTAKATIFU²⁴ na ya kuwa ameketi upande wa kuume wa MUNGU kwa wakati huu akisikilia za maungamo ya dhambi zangu na maombi yangu haya.²⁵ Ninafungua mlango wa moyo wangu na kukaribisha moyoni mwangu, BWANA YESU.²⁶ Nioshe dhambi zangu kwa damu uliyoimwaga kwa ajili ya nafsi yangu pale msalabani Kalivari,²⁷ huta-

nikataa, BWANA YESU, utanisamehe dhambi zangu na kuiokoa roho yangu. Ninalijua hili kwa sababu NENO LAKO, yaani Biblia linasema hivyo.²⁸ NENO LAKO linasema hutamkataa ye yote na mimi nikiwemo.²⁹ Hivyo ninajua kwamba umenisikia, na ya kuwa umenijibu; na ninafahamu kwamba nimeokoka.³⁰ Ninakushukuru BWANA YESU kwa kuokoa roho yangu na nitaonyesha shukrani zangu kwa kufanya yale unayoniamuru na kwa kutotenda dhambi tena.³¹

Sasa kwa kuwa umeokoka, mtumikie MUNGU kwa moyo wako wote, roho yako yote, akili zako zote na kwa nguvu zako zote (Marko 12:30).³² Ubatizwe kwa kuazamishwa kwenye maji, kwa jina la BABA, la MWANA, na la ROHO MTAKATIFU.³³ Kwa bidii soma Biblia Takatifu (tolo la The Bible League – Waenezaji wa Neno la MuNGU TANGU 1938) na ufanye kile isemacho mpaka siku utakayokufa.³⁴

Basi, kama YESU alivyoamuru, umshindie roho. Unaweza kufanya hivyo kwa kuwa msambazaji wa Maandiko ya Mchungaji Alamo. Tunachapa maandiko ya Mchungaji Alamo katika lugha nyingi, na tunayapeleka ulimwenguni

kote. Tunatumia mamilioni ya dola kunnua karatasi na usafirishaji, hivyo tunahitaji maombi yenu na msaada wa kifedha.

Iwapo unataka dunia yote iokolewa, kama YESU anavyoamuru, basi usimwibie MUNGU zaka na sadaka zake. MUNGU alisema, “Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mmaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekubia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote [na dunia hii yote]. Leteni zaka [zaka ni asilimia 10 ya mapato yako yote] kamili ghalani, ili kiwemo chakula [chakula cha kiroho] katika nyumba yangu [roho zilizookolewa], mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea ye ye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi” (Malaki 3:8-12).

²¹ Zab. 51:5, Rum. 3:10-12, 23 ²² Mat. 26:63-64, 27:54, Lk. 1:30-33, Yoh. 9:35-37, Rum. 1:3-4 ²³ Mdo. 4:12, 20:28, Rum. 3:25, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 5:9 ²⁴ Zab. 16:9-10, Mat. 28:5-7, Mk. 16:9, 12, 14, Yoh. 2:19, 21, 10:17-18, 11:25, Mdo. 2:24, 3:15, Rum. 8:11, 1 Kor. 15:3-7 ²⁵ Lk. 22:69, Mdo. 2:25-36, Ebr. 10:12-13 ²⁶ 1 Kor. 3:16, Ufu. 3:20 ²⁷ Efe. 2:13-22, Ebr. 9:22, 13:12, 20-21, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 1:5, 7:14 ²⁸ Mat. 26:28, Mdo. 2:21, 4:12, Efe. 1:7, Kol. 1:14 ²⁹ Mat. 21:22, Yoh. 6:35, 37-40, Rum. 10:13 ³⁰ Ebr. 11:6 ³¹ Yoh. 5:14, 8:11, Rum. 6:4, 1 Kor. 15:10, Ufu. 7:14, 22:14 ³² Mat. 28:18-20, Yoh. 3:5, Mdo. 2:38, 19:3-5 ³³ Kumb. 4:29, 13:4, 26:16, Yos. 1:8, 22:5, 2 Tim. 2:15, 3:14-17, Yak. 1:22-25, Ufu. 3:18

Tafadhalii wasiliana nasi kwa habari zaidi au kwa vitabu vyetu vyenye mada nyininge ambazo unaweza kuvutiwa nazo:

**Tony Alamo, World Pastor, Tony Alamo Christian Ministries Worldwide • P.O. Box 2948, Hollywood, CA 90078
Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni: (661) 252-5686 • Faksi: (661) 252-4362**

www.alamoministries.com • info@alamoministries.com

Huduma ya Tony Alamo Christian Ministries Worldwide hutoa mahali pa kuishi pamoja na vitu vyote muhimu kwa maisha kwa wale walio Marekani ambao wanataka kumtumikia BWANA kwa miyo yao yote, roho zao zote na nguvu zao zote.

Huduma yetu hufanyika jijini New York kila Jumanne, saa mbili usiku na mahali pengine kila usiku.

Tafadhalii wasiliana nasi kuitia simu namba (908) 937-5723 kwa habari zaidi. CHAKULA HUTOLEWA BAADA YA KILA IBADA.

Tuma maombi ujipatie kitabu cha Mchungaji Alamo kiitwacho, The Messiah, kinachomwonesha KRISTO
alivyo katika Agano la Kale kwa jumbe za unabii zipatazo 333.

Kuwa mmoja wa watumishi katika kuvuna roho za watu kwa kuwa msambazaji wa makala na vitabu vya Mchungaji Alamo
Machapisho yetu na jumbe kwenye tepu za sauti hayalipishwi kitu ikiwemo gharama ya kusafirisha kupitia meli.

Iwapo kuna mtu atajaribu kukulipisha, tafadhalii tupigie simu kwa namba: (661) 252-5686.

**MAKALA HIZI ZIMEBEBA MPANGO WA KWELI WA UKOMBOZI (Matendo ya Mitume 4:12)
USIZITUPE: ZIFIKISHE KWA MTU MWINGINE.**

**Kwa wale ambao mko kwenye nchi nyininge, tunawashauri kutafsiri makala hizi kwa lugha zenu. Iwapo
mtachapisha tena, tafadhalii jumuisha haki hii na usajili:**